



Mafundisho na Maagano 76

JULAI 5-11

Kusikia kuhusu Daraja Tatu za Utukufu kwa Mara ya Kwanza

Sehemu ya 76 ya Mafundisho na Maagano inafafanua vipengele muhimu vya mpango wa wokovu ambavyo vilipotea kutoka duni-ani wakati wa ukengeufu. Kwa watu wengi, kujifunza kweli hizi zilizorejeshwa kwa mara ya kwanza ni uzoefu wa kukumbukwa. Hii ilikuwa kweli kwa **Connie, mwongofu kutoka Richmond, Virginia, MAREKANI.**

Anakumbuka: "Siku zote nimeona upendo wa Mungu wakati ninaposoma Biblia, bali kamwe sikuweza kupata kanisa lolote ambalo lilifundisha kwa njia niliyoielewa. Wakati nilipopata somo la wamisionari juu ya mpango wa wokovu, nilijihisi kuthibitishiwa na amani kama ambavyo kabla sijaisikia kamwe. Nilijifikiria mwenyewe, 'Huyo ni Baba wa Mbinguni ninayemjua.' Kujifunza kuhusu madaraja ya utukufu kulifungua akili zangu kwa mapana sana kiasi kwamba sikuweza kuzuia msisimko wangu wa kujifunza zaidi."



**Delphine, mwo-
ngofu kutoka Paris,
Ufaransa,** ana hali ngumu ya kifamilia, kwa hiyo wakati wamisionari walipomfundisha kwa-mba familia zinaweza kuishi pamoja katika ufalme wa selestia, hakuwa na uhakika kama ni kitu anachokitaka. Wakati wamisionari walipoendelea kumfundisha kuhusu daraja tatu za utukufu, hata hivyo, alipata faraja. Alijifunza kwamba ataweza kuwa na wale anaowapenda waliochagua kuifuata injili. Pamoja na uelewa mzuri sana wa mpango wa wokovu, alisema, "niliona ni haki kabisa na hiyo ilinihakikishia."

MJADALA

Ni baadhi ya kweli zipi kutoka sehemu ya 76 ambazo zinakutia hamasa kuwa unayestahili kwenye ufalme wa selestia?